# Urithi WETU

# Samia anavyoirejesha Kilwa katika ramani ya dunia










Na Immaculate Makilika - Maelezo

KILWA ina historia kubwa katika Tanzania na dunia nzima kabla, wakati wa harakati na baada ya Uhuru wa nchi mwaka 1961.

Eneo hilo lililokuwa maarufu pia kwa biashara ya utumwa kabla ya Uhuru, lina mchango mkubwa katika harakati za kutafuta uhuru na kukuza uchumi kupitia utalii.

Moja ya eneo lenye mchango mkubwa ni Bandari ya Kilwa iliyopo mkoani Lindi, ambayo imekuwa ikitumika zaidi kwa shughuli za utalii na kwa kiasi kidogo shughuli za uvuvi.

Kwa kuwa mkakati wa serikali ni kukuza sekta za uvuvi na utalii nchini, imeanza kutekeleza mradi wake wa kimkakati wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa, sambamba na kusaidia wananchi kunufaika na rasilimali za bahari.

Akizungumza wilayani Kilwa eneo la Kilwa Masoko wakati akiweka jiwe la msingi katika Bandari ya Uvuvi Kilwa na kugawa boti za kisasa 160 kwa wavuvi, ikiwa ni mradi wenye thamani zaidi ya Sh bilioni 280, Rais Samia Suluhu Hassan

Inaendelea Uk. 13

HABARI LEO UK 13

# Samia anavyoirejesha Kilwa katika ramani



Inatoka Uk. 9

amesema serikali imefanya tukio muhimu la kihistoria kwa kujenga bandari hiyo ya kwanza ya uvuvi nchini.

"Boti hizi 160 zimetolewa kwa mkopo wa masharti nafuu na unalenga kutoa ajira na kuongeza kipato cha jamii. Boti ndogo zitatumiwa na akina mama kulima mwani na kubeba mizigo, na zile kubwa zinakwenda kwenye kina cha maji marefu," anasema Rais Samia.

Rais Samia anasema serikali haitarajii boti hizo kuleta ugomvi katika vikundi vya wakulima na wavuvi bali ziimarishe uchumi wao.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega anasema katika boti hizo zipo ndogo na zenye ukubwa wa mita 14 na uwezo wa kuhifadhi samaki hadi tani 1.5.

"Tunamshukuru Rais kwa kutupa fedha shilingi bilioni 11.5 zitakazowasaidia wavuvi na kazi imeanza. Leo unajenga bandari ya kwanza ya wavuvi, bandari hii inakwenda kuinua uchumi kupitia sekta ya uvuvi kutoka asilimia 1.8 hadi 10 kufikia mwaka 2036, hiyo itawezekana kwa kuwakaribisha wawekezaji wakubwa duniani," anaeleza Ulega.

**Manufaa Bandari ya Uvuvi Kilwa**

Anasema bandari hiyo itakuwa na karakana ya meli, sehemu ya kuegesha meli kubwa kumi zenye urefu wa mita 30. Aidha, meli kutoka maeneo mbalimbali duniani zitaweza kuweka nanga pamoja na shughuli mbalimbali zitakazofanyika ikiwemo kuongeza chumvi kwenye samaki kabla ya kusafirisha.

Manufaa mengine ya bandari hiyo ni uwezo wa kuhifadhi boti ndogo, sehemu ya kuegesha mitumbwi isiyopungua 200, sehemu ya kuegesha mashua na kutoa fursa ya kutoa ajira kwa vijana takribani 30,000.

"Pia, bandari hii itakuwa na uwezo wa kuhifadhi samaki tani 1,300 kwa wakati mmoja, soko la samaki litakalotumika na wavuvi katika ukanda wa Kusini na eneo la kuchakata samaki," amesisitiza Waziri Ulega.

Aidha, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa bandari hiyo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) itaendesha shughuli za bandari hiyo kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mnufaika wa mradi huo, Shukrani Shamte ambaye ni mkulima wa mwani ameipongeza serikali kwa jitihada hizo.

"Tunashukuru serikali kwa kutupatia mkopo wa boti ya malipo nafuu, boti hizi zitatusaidia kwenye shughuli za kulima mwani kwenye kina cha maji mengi na kubeba mwani kutoka kwenye maji mengi kuja pwani.

"Wakulima wengi wa mwani tunaomba utuwezeshe boti zingine na mahitaji ni mengi na boti ulizotupa ni chache," anaeleza Shukrani.

HABARI LEO UK 19

# Polisi kula sahani moja na wavuvi haramu

Na Lucy Ngowi

KAMANDA wa Polisi Kikosi cha Wanamaji Tanzania, Moshi Sokoro amesema wataendelea kupambana na uvuvi haramu wa kutumia baruti na kokoro ili kutimiza azma ya serikali ya kuwa na uchumi wa buluu endelevu.

Akizungumzia athari za uvuvi haramu hapa nchini alisema: "Kama rais (Samia Suluhu Hassan) anavyosema tuko katika uchumi wa buluu sasa tutaingiaje uchumi wa buluu huku tunafanya uvuvi haramu? Hiyo haiwezekani."

Aliagiza wavuvi kufuata sheria, kanuni na uvuvi salama na kuachana na uvuvi haramu ambao una athari kwa walaji wa samaki.

Alisema katika kusimamia uvuvi haramu, kuanzia miaka 2022 na 2023, tayari watuhumiwa 17 wameshakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Alisema watuhumiwa hao wamefanya makosa 11 ambayo baadhi ya makosa yametolewa uamuzi na watuhumiwa kulipa faini mahakamani, mengine majalada yapo chini ya upelelezi.

"Makosa mengi ambayo yameorodheshwa ni ya uvuvi haramu wa kutumia kokoro zile nyavu ndogo ndiyo ambayo yanaonekana kuwa mengi katika ukamataji wetu," alisema na kuongeza kuwa mengine ni ya uvuvi wa kutumia baruti.

